

9

## MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI (VETA)

### MKATABA WA UJENZI

Mkataba huu umesainiwa leo tarehe 22 mwezi 03 2022

#### KATI YA

Chuo cha Ufundi Stadi (na Huduma) cha MPANDA, S.L.P. 190,  
MPANDA ambacho kinaiwakilisha Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya  
Ufundi Stadi, S.L.P. 2849 Dar es Salaam (ambacho katika Mkataba huu atajulikana  
kama "Mwajiri") kwa upande mmoja;

NA

KELVIN N. MEELA S.L.P. 40, MPANDA  
(ambaye katika Mkataba huu atajulikana kama "Fundi") kwa upande mwingine

KWA KUWA Mwajiri ana mpango wa kujenga Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya  
CHUNYA ;

KWA KUWA Mwajiri anatumia rasilimali zake za ndani kwa ushirikiano na rasilimali za  
nje kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Ufundi Stadi cha Wilaya ya CHUNYA ;

KWA KUWA Mwajiri amefanya majadiliano na Fundi kwa ajili ya kazi ya  
KUWEKA JAKAFI YA MARUMARU NA KUPATA RAXGI BWENI LA WAWULANI

NA KWA KUWA Mwajiri amempatia Fundi nakala ya Michoro pamoja na Mchanganuo  
wa vifaa vya Ujenzi (*Schedule of materials*) vinayoonesha namna kazi itakavyofanyika;

#### HIVYO BASI, PANDE ZOTE MBILI ZINAKUBALIANA KAMA IFUATAVYO:

##### 1. GHARAMA YA UFUNDI

Kwamba, kwa gharama ya Shilingi za Tanzania 7,580,000, Fundi  
atafanya kazi ya MARUMARU NA RANGI kwa masharti yaliyo katika Mkataba huu.  
Katika Mkataba huu, kiasi hiki cha fedha kitajulikana kama "Gharama ya Ufundi"

## **2. MABADILIKO YA GHARAMA YA UJENZI (CONTRACT SUM ADJUSTMENT)**

Gharama ya ufundi haitabadilika kwa namna yoyote ile isipokuwa itakapokuwa imeelekezwa moja kwa moja katika Mkataba huu kutokana na mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri.

## **3. NAMNA YA KUFANYA MALIPO**

Mwajiri atamlipa Fundi kwa hundi ndani ya siku kumi na nne kwa namna ifuatayo;

- (a) Malipo ya awali, 10 % ya gharama ya ufundi
- (b) Kazi ikikamilika kwa asilimia 20: 15% ya Gharama ya Ufundii;
- (c) Kazi ikikamilika kwa asilimia 50: 20% ya Gharama ya Ufundii;
- (d) Kazi ikikamilika kwa asilimia 80:30% ya Gharama ya Ufundii;
- (e) Kazi ikikamilika kwa asilimia 100: 20% ya Gharama ya Ufundii;na
- (f) Baada ya kukamilika kwa "Muda wa matazamio":5% ya Gharama ya Ufundii.

## **4. MAKABIDHIANO YA ENEO LA KAZI, UKAMILISHAJI WA KAZI NA KUAHIRISHA KAZI**

- (a) Fundi atakabidhiwa eneo la tarehe 25 mwezi 03 2022 au tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa. Iwapo Fundi atakabidhiwa tarehe nyingine kabla au baada ya tarehe tajwa, pande zote zitaweka kumbukumbu kwa maandishi siku ya makabidhiano ambapo pande zote mbili zitasaini.

- (b) Fundi atakamilisha kazi ndani ya siku 25 toka tarehe ya makabidhiano ya kazi hiyo. Iwapo kutatokea mabadiliko ya ujenzi yaliyofanywa na Mwajiri, siku ya ukamilishaji wa ujenzi inaweza kubadilika.

- (c) Mwajiri anaweza kuahirisha kazi zilizo katika Mkataba huu na kutoa maelekezo kwa Fundi kuhusiana na kuahirisha kazi hiyo.

## **5. WAJIBU WA FUNDI**

Fundi atakuwa na wajibu ufuataao: -

- (a) *ya marumaru na kupaka rangi*  
Kuweka Takafu na kukamilisha kazi kama inavyoonekana katika Michoro pamoja na Mchanganuo wa Vifaa vya Ujenzi (*Schedule of materials*) sambamba na maelekezo ya Mwajiri;
- (b) Kumpatia Mwajiri ratiba ya kazi (*work programme*)ndani ya siku 7 tangu tarehe ya kusaini Mkataba huu ili kupata kibali cha Mwajiri.

IMESAINIWA NA KUWEKWA MHURI, KWA NIABA YA MAMLAKA YA ELIMU NA  
MAFUNZO YA UFUNDI STADI, NA CHUO CHA UFUNDI STADI (NA HUDUMA) CHA

ZIPANDA

Jina: Tastua Ndzane Saini:

Thiagore

Wadhifa: MKUU WA CHUO Tarehe:

22/03/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: ERASmus ZUMBA Saini:

E.

Wadhifa: Mwanzu Tarehe:

22/03/2022

IMESAINIWA NA FUNDI

Jina: Kelvin M. Meela Saini: Mbele ya

Kelvi

Wadhifa: FUNDI Tarehe:

22/03/2022

Mbele ya (Shahidi)

Jina: Stephano Kamibumba Saini:

Step

Wadhifa: Fundi Tarehe:

22/03/2022